

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE

23 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI NA NNE – TAREHE 23 JUNI, 2023

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**704. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU
(KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Zahanati 18 katika Tarafa za Laela, Mpui, Mtowisa na Kipeta.

**705. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua changamoto ya upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Vijijini.

**706. MHESHIMIWA JACKSON GEDION
KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara kutoka Kijiji cha Kalenga kupitia Kata za Ulanda, Maboga, Wasa - Madibila zitapandishwa kuwa za Mkoa.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**707. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI
(MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga mitaro ya kuchepusha maji katika Kata za Bulyanghulu, Segese, Ngayana Bulige.

**708. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Mpanda hadi Uvinza yenye Km 159 utakamilika.

709. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Mbuguni kuanzia Tengeru Sokoni, Arumeru hadi Mererani utaanza.

WIZARA YA AFYA:

710. MHESHIMIWA BENARDETHA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutokomeza kabisa ugonjwa wa Malaria nchini.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

711. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inatumia utaratibu gani kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mipango na Bajeti zinazopitishwa.

712. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini mianya ya majadiliano yanayopelekea rushwa kwenye mfumo wa ukadiriaji wa kodi kwa Wafanyabiashara itaondolewa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

713. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARABI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Mji Mdogo wa Ngaramtoni.

WIZARA YA KILIMO:

714. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali italetwa Bungeni Muswada wa Sheria wa kulinda ardhi ya Kilimo.

WIZARA YA NISHATI:

715. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka Umeme wa REA katika Vijiji na Vitongoji ambavyo vimeshawekewa nguzo Jimbo la Rungwe.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

716. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, nini mkakati wa kuongeza nguvu kwenye Uvuvi ili Vijana wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa wanufaike na Ziwa Victoria.

717. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Mwaka 2021 - Januari 2022 Sekta ya Mifugo imeuza nyama nje ya nchi kwa asilimia ngapi na upi mkakati wa kuimarisha Sekta hii.

WIZARA YA MADINI:

**718. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO
(BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, lini Serikali italeta maboresho ya Sheria ya Madini ili Wananchi wanufaike na rasilimali zilizopo katika maeneo yao.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
23 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**